

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**



**SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**Kumb. Na EA.7/96/01/ K/243**

**24, Julai, 2020**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya **Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi moja **(01) kama ilivyoainishwa hapa chini.**

**1.0 MSAIDIZI WA MAKTABA DARAJA LA II: (NAFASI 1)**

**1.1 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kuandikisha wasomaji;
- ii. Kupanga vitabu katika rafu (shelves);
- iii. Kuazimisha na kupokea vitabu vilivyoazimwa;
- iv. Kukarabati vitabu vilivyochakaa; na
- v. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wa Kazi.

**1.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye Cheti cha Mthani wa Taifa wa Kidato cha IV ambao wamefaulu Mafunzo ya Wasaidizi wa Maktaba (Library Assistants Certificates Course) yanayotolewa na Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania au wenye Cheti kinacholingana na hicho kutoka kwenye Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi ya mshahara wa Ofisi ya Bunge **PSS B**

#### **MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. **Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishie barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao.**
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya Wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
  - Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates.
  - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
  - Computer Certificate
  - Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)
  - Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni.
- vi. **Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- vii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).**
- viii. Waombaji wa nafasi za Ajira waliostaafishwa/kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- ix. Waombaji kazi ambao tayari ni Waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahasika watachukuliwa hatua za kisheria.

- xi. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 06 Agosti,2020**
- xii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA**

xiii. *Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo;*

<http://portal.ajira.go.tz/>

(Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa '*Recruitment Portal*')